

*Utenzi ufuatao uliandikwa na Mshairi Hamidu R. Tambwe kwa baba yake Rajabu Saleh Tambwe akisisitiza kupata majibu ya utenzi wake ambao aliuandika kwa baba yake na umechapishwa kwenye Diwani ya Tanzanet Toleo #2. Lengo la shairi lake ilikuwa ni kumkumbusha Mshairi Marehemu Rajabu S. Tambwe kwenda kutimiza moja ya nguzo za dini yake, ambayo ni kwenda hija.*

**RAJABU SALEH TAMBWE**

- |  |   |  |
|--|---|--|
| 1. Mheshimiwa Rajabu,<br>Haki naona ajabu,<br>Kutokupata majibu,<br>Ya hizo zangu nyaraka.   | 4. Mimi naona ajabu,<br>Kwa mtu kama Rajabu,<br>Wazikataa thwababu,<br>Kama aliye zuzuka!     | 7. Kwako huo ni wajibu,<br>Utende bila sulubu,<br>Tena bila ya ghadhabu,<br>Muhibu hayo pulika.  |
| 2. Mimi yangu maarubu,<br>Ni kuwa wewe muhibu,<br>Wende Makka ughaibu,<br>Hijja uende iweka. | 5. Mzungupule Rajabu,<br>Usiye na masaibu,<br>Yote hayo matilabu,<br>Unayo pasina shaka.      | 8. Ninajua sikukugubu,<br>Wala sikukughilibu,<br>Ila nilikukhatibu,<br>Kuwa baba nenda Makka.    |
| 3. Wewe ni wangu sahibu,<br>Budi nikupe jawabu,<br>Nenda huko taratibu,<br>Uende kutakasika. | 6. Kwetu wewe mahabubu,<br>Tukupendaye ajabu,<br>Hapana wa kukusibu,<br>Kisamba haya kumbuka. | 9. Lau kama unaona,<br>Kuwa wewe fedha huna,<br>Mimi kusoma natakana,<br>Ili baba wende Makka.   |
|  |   | 10. Mengi sintayatongoa,<br>Abu wangu kukwambia,<br>Hayo yote watambua,<br>Tena bila ya mashaka. |

*Hamidu R. Tambwe  
MBEYA,  
Februari, 1968.*